**HOTUBA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA BWANA GEORGE D. YAMBESI KUMKARIBISHA KATIBU MKUU KIONGOZI BALOZI OMBENI Y. SEFUE KWENYE UZINDUZI WA WAKALA ZA SERIKALI TAREHE 11 JULAI, 2012**

***Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;***

***Ndugu Makatibu Wakuu na;***

***Naibu Makatibu Wakuu;***

***Watendaji Mbalimbali wa Serikali;***

***Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Ushauri za Wizara mliopo;***

***Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali;***

***Wakurugenzi;***

***Ndugu Wanahabari;***

***Wageni Waalikwa;***

***Mabibi na Mabwana.***

Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kukukaribisha Katibu Mkuu Kiongozi katika hafla hii ya uzinduzi wa Wakala tano za Serikali ambazo ni: Wakala ya Serikali Mtandao; Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao; Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi; Wakala ya Mafunzo ya Mifugo na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania. Kwa namna ya pekee napenda nikushukuru sana kwa kukubali kwako kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huu wa taasisi hizi muhimu za

Serikali, licha ya majukumu yako makubwa uliyonayo ya Kitaifa. Pili, napenda kuwashukuru wageni wetu wengine wote mliopo hapa kwa kutenga muda wenu ili kuhudhuria hafla hii. Nasema asanteni na karibuni sana.

***Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wakala na Wageni Waalikwa;***

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kama msimamizi mkuu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245, imeendelea kuziwezesha Wizara mbalimbali katika mchakato wa kubadili baadhi ya majukumu ya Idara na Vitengo vyao kuwa Wakala za Serikali, ili zifanye kazi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na tija zaidi. Tukio la leo ni ushahidi wa mchakato huo na linatufanya tufikishe jumla ya Wakala thelathini na tano (35) tangu mpango huu ulipoanzishwa mwaka 1999. Wakala hizi zinatakiwa kutumia mbinu za kisasa kiutendaji na za kiuendeshaji ili kuboresha zaidi utendaji kazi na kutoa huduma bora, kwa kiwango na kwa wakati lakini zikiwa kwenye uangalizi wa karibu wa Serikali. Hii inatukumbusha ile dhana maarufu ya **‘ Eyes On, Hands Off’.**

***Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi na Wageni Waalikwa;***

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU), ambayo imepewa jukumu la kuwezesha uanzishwaji wa Wakala za Serikali, imeendelea kutekeleza jukumu hilo huku ikijenga uwezo wa wataalam wa ndani. Nafurahi kusema kuwa Wakala zote unazozizindua leo ni matunda ya juhudi hizo kwa sababu zimewezeshwa kwa kutumia wataalam wa ndani badala ya wataalamu wa nje kitu ambacho kimeokoa fedha nyingi za Serikali.

Ndugu Mgeni rasmi, haya yote yamefanikiwa kutokana na ushirikiano mkubwa kutoka kwa Wizara mama za Wakala. Naomba kipekee kumshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Menejimenti yake ambao nao leo wanazindua Wakala za Serikali tatu pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara nyingine zote kwa ushirikiano wao katika mchakato mzima wa uanzishaji Wakala za Serikali. Niwaombe ushirikiano wao zaidi katika kusimamia, kuzijengea uwezo na kuziimarisha kiutendaji Wakala zote tunazozianzisha ili zizidi kuboresha utoaji wa huduma zao.

***Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;***

Kama nilivyoeleza hapo awali, leo hii utatuzindulia rasmi Wakala tano ambazo mbili ziko chini ya Ofisi yangu, ambazo ni Wakala ya Serikali Mtandao na Wakala

ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao. Wakala zingine tatu ziko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi nazo ni Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi; Wakala ya Mafunzo ya Mifugo na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania. Kwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi atatoa maelezo mafupi juu ya Wakala zilizo chini ya Wizara yake naomba nitumie nafasi hii kueleza machache juu ya Wakala zilizo chini ya Ofisi yangu.

***Ndugu Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;***

Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao *(Tanzania Global Learning Agency-TaGLA),* imeanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245 na Tangazo la Serikali No.425 la tarehe 23 Desemba, 2011. TaGLA inachukua majukumu ya kilichokuwa Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia *(Tanzania Global Development Learning Centre –TGDLC),* kilichoanzishwa mwaka 2000 kama sehemu ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma. TaGLA itatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia kasi ya ukuaji wa teknolojia hapa nchini na duniani kote kwa kujenga uwezo wa Watanzania, na hasa watumishi wa Umma, kwa kutumia teklolojia mbalimbali. Mojawapo ni matumizi ya teknolojia ya ‘*video conference*’, inayowezesha kufanya mafunzo, kubadilishana mawazo kwenye midahalo, kupata nafasi ya kushiriki makongamano ya kitaifa na kimataifa na kuweza kufanya maamuzi yenye

ufahamu wakati wote kwa kuunganishwa na wataalam mbalimbali waliopo nje ya nchi, na kokote duniani.

***Mhe. Mgeni rasmi;***

Uzoefu umeonesha kuwa teknolojia hii imeweza kutoa mchango mkubwa wa kuendesha mafunzo ya Uongozi, Utawala Bora, Jinsia, Kilimo na Masoko, Afya, Mazingira, Matumizi ya Teknolojia na stadi nyingi zinazoboresha ueledi wa watendaji Serikalini na katika sekta binafsi. Pia tumeshuhudia njia bunifu za kiutendaji zilizoweza kutumia teknolojia hii na kuokoa fedha nyingi za Watanzania ikiwemo kuendesha kesi mahakamani na kuleta mashahidi kwa teknolojia ya 'video conference', kufanya usaili, kudahili waombaji kazi na kuchambua mikataba mbalimbali kabla ya kuidhinisha.

***Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;***

Wakala ya Serikali Mtandao (e-Government Agency-eGA) kwa upande wake imeanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245 na Tangazo la Serikali No 494A la tarehe 17 Desemba, 2010. Wakala hii ina jukumu la kuandaa na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuweza kuboresha huduma zinazotolewa na Serikali kwa wananchi kwa kutumia teknolojia mbalimbali. Ni mategemeo yangu

kwamba Wakala ya Serikali Mtandao itatupatia ufumbuzi wa kero nyingi za kiutendaji Serikalini na wananchi kwa ujumla katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa wakati, na karibu zaidi na Wananchi.

Kwa mantiki hiyo, ujio wa Wakala ya Serikali Mtandao utakuwa ni jibu muafaka katika kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma mbalimbali Serikalini. Wakala hii itatoa huduma ambazo ni mtambuka kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuleta ufanisi na matumizi bora ya TEHAMA, huku ikipunguza gharama za uendeshaji kwa Serikali katika uwekezaji kwenye eneo la TEHAMA. Ni mategemeo yangu pia kwamba Wakala hii itabuni njia rahisi za kufikisha huduma kwa wananchi ikiwemo matumizi ya simu za kiganjani, tovuti na barua pepe.

***Mhe. Mgeni rasmi, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wakala na Wageni Waalikwa;***

Tunao uhakika kwamba teknolojia inatupa nafasi nzuri ya kuweza kuboresha uwajibikaji, uwazi na ufanisi Serikalini na hivyo kuongeza kasi ya kufanya maamuzi na kutoa taarifa kwa wananchi kwa wakati. Kuwepo kwa teknolojia rafiki hapa nchini kunatoa nafazi nzuri kwa Wakala hizi unazozizindua leo

kufikia lengo hilo.

***Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;***

Nimalizie kwa kukushukuru tena wewe binafsi kwa msaada na maelekezo mbalimbali unayotupatia kupitia Ofisi yako, katika kuhakikisha Serikali inasimamia vizuri utoaji wa huduma kwa Umma wa Watanzania. Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika maandalizi ya uanzishwaji na uzinduzi wa Wakala hizi, na kwa wote mliokuja kushiriki katika tukio hili muhimu.

Napenda sasa nikuombe Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi ukabidhi rasmi Nyenzo za Utendaji Kazi kwa Watendaji Wakuu wa Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) ambazo zipo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ishara ya kuziagiza kuanza kutekeleza majukumu yao rasmi.

***Asanteni sana kwa Kunisikiliza***